# HALMASHAURI YA MJI KOROGWE
# SHULE YA SEKONDARI KILOLE DAY

S.L.P 678,
KOROGWE.
20/12/2020

SIMU: **0714497071-MKUU WA SHULE**
**0653577977-MAKAMU MKUU WA SHULE**

**Kumb. Na. KLSS.2119/J/1/2020/0001**
**JINA LA MWANAFUNZI:..........................................**

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KILOLE DAY WILAYA YA KOROGWE MWAKA 2021

1. Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza (I) shule ya sekondari ya kutwa Kilole Day Mwaka 2021. Shule hii ipo Kata ya Kilole, Halmashauri ya Mji wa Korogwe. Ukitoka Korogwe Mjini kuelekea Tanga, shule ipo upande wa kushoto wa barabara kuu karibu na Hoteli ya Highway (Dar- Express).
   Shule itafunguliwa Tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni Tarehe 20/01/2021.

2. **Sare za shule:**
   a) **Wavulana**
      i. Suruali mbili rangi ya kijivu mpauko. Upana miguuni inchi 16-17.
      ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi.
      iii. Viatu vya ngozi vya rangi nyeusi jozi mbili. Viatu viwe vya kufunga kamba na visiwe na visigino virefu.
      iv. Soksi ndefu za rangi nyeusi.

   b) **Wasichana**
      i. Sketi mbili rangi ya kujivu mpauko. Sketi ziwe ndefu zinazofunika soksi.
      ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi au nusu kanzu mbili zenye mikono mirefu na hijabu mbili nyeupe.
      iii. Viatu vya ngozi vya rangi nyeusi jozi mbili. Viatu viwe vya kufunga kamba au visiwe vya kufunga kamba (Juma na Roza); na visiwe na visigino virefu.
      iv. Soksi ndefu za rangi nyeupe.

   c) Sweta rangi ya kijivu lenye mikono mifupi kwa wanafunzi wote.
   d) Track ya bluu na T-shirt ya bluu kwa ajili ya michezo kwa wanafunzi wote.

3. **Vifaa vya kujifunzia:**
   a) Madaftari kumi (10) (counter books quire 2/3).
   b) Kalamu za wino na penseli za kutosha.
   c) Mkebe (Mathematical set).
   d) Kamusi ya Kingereza –Kingereza.
   e) Vitabu vya masomo ya sekondari kidato cha kwanza kulingana na uwezo wa mzazi.
   f) File la kutunza kumbukumbu za mitihani.

4. **Vifaa vya usafi**
   Kila mwanafunzi wa kidato cha I anatakiwa aje na vifaa vifuatavyo:
   a) Ufagio wa chelewa.
   b) Jembe jipya lenye mpini
   c) Ndoo mpya ya plastiki ya lita 10.
   d) Fyekeo jipya lililonolewa.

5. **Huduma ya afya**
   Kila mwanafunzi ambaye hana kadi ya NHIF anatakiwa kujiunga na mfuko wa CHF ili apate matibabu pindi atakapougua.
6. **Huduma ya chakula**
   Huduma ya chakula shuleni ni muhimu; itatolewa kwa utaratibu utakaopatikana shuleni baada ya kikao cha wazazi.
7. **Sheria za shule**
   a) **HESHIMA:** Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na heshima kwa watu wote; wakubwa kwa wadogo. Wanapoona watu wakubwa wawasalimu kwa heshima wakiwa wamesimama. Wawapokee wageni wanaofika shuleni na kuwapeleka sehemu husika.
   **NB.** Kama mgeni/mwalimu amebeba mzigo mwanafunzi hana budi kupokea mzigo na kuupeleka mgeni/mwalimu anapokusudia.
   b) **MAHUDHURIO:** Wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria shuleni na madarasani siku zote za masomo bila kukosa.
   c) **KUWAHI SHULE:** Wanafunzi wote wanatakiwa kuwahi shuleni mapema asubuhi. Wawahi namba na kufanya usafi maeneo waliyopangiwa.
   d) **SARE ZA SHULE:** Wanafunzi wote wanatakiwa kuvaa sare za shule muda wote wawapo shuleni. Wanafunzi wavulana wasivae suruali **modo** na wasichana wasivae sketi fupi na zinazobana.
   e) **USAFI:** Wanafunzi wote wanatakiwa kuzingatia usafi wa mwili, mavazi na mazingira.
   f) **MSUKO**: Wanafunzi hawaruhusiwi kusuka aina yeyote ya msuko.
   g) **KELELE**: Ni marufuku wanafunzi kupiga kelele katika mazingira ya shule; iwe ni darasani au nje ya darasa.
   h) **MIPAKA YA SHULE**: Wanafunzi wote hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo/mapumziko ispokuwa kwa kibali maalum.
   i) **MATEMBEZI**: Wanafunzi wote hawaruhusiwi kutembelea vilabu vya pombe, nyumba za starehe na nyumba za kufikia wageni.
   j) **MICHEZO**: Wafunzi wote wanatakiwa kushiriki katika michezo mbali mbali shuleni
8. **Makosa yanayoweza kumfukuzisha mwanafunzi shule**:
   a) Wizi
   b) Uasherati
   c) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na bangi, cocaine, mirungi, kuberi nk.
   d) Kupiga au kupigana.
   e) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma aumma au ya mtu.
   f) Kudharau bendera ya Taifa.
   g) Kuoa au kuolewa.
   h) Kupata, kutoa, kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
   i) Kugoma au kuchochea/kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
   j) Kukataa au kugomea adhabu.
   k) Kumiliki au kukamatwa na simu ya mkononi.
9. Mambo mengine
   a) Kila mwanafunzi lazima apimwe afya na Mganga wa Hospitali ya serikali kwa kutumia fomu maalum (Kiambatisho A). Fomu hii iletwe shuleni mwanafunzi atakaporipoti.
   b) Kila mwanafunze ajaze KIAMBATISHO B; na mzazi/mlezi wa mwanafunzi ajaze KIAMBATISHO C.

……………….
JUMAA K. HASSANI

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KILOLE
KOROGWE

**KIAMBATISHO A**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A**

TO: Medical Officer
……………………………………..
……………………………………..
……………………………………..

From
………………………………………
………………………………………
………………………………………..

Mr./Mrs./Ms…………………………………………………………..
(Name in full)

Please examine the above named to his/her physical and mental fitness for secondary education course. The examination should include categories I-IV in which each category or sub-category will render the student in ineligible in of defect.

Date …………………………. Signature……………………

**PART B**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined above named and consider that he/she is physically benefited and mentally fit/unfit for secondary education course.

I

a) Eyesight ………………………..……..
b) Hearing ……………………..……...
c) Limb ……………………………..……
d) Speech ……………………….….…
e) Venereal disease……………………
f) Leprosy ……………………………
g) Epilepsy ……………………………
h) Typhoid …………………………….

II Neurosis ………………………………...

III Other serious diseases……………………………………………………………………...
…………………………………………………………………………………………………..

IV Pregnancy………………………………..

Date ………………………. Signature……………………
Station …………………… Designation………………..

**KIAMBATISHO B (Jaza na irudi shuleni)**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KUJIUNGA NA SHULE**

1. Mimi ..................................................nimesoma maagizo,sheria pamoja na taratibu za kujiunga na shule
2. Ninaahidi kutimiza maagizo yote yaliyopo katika barua ya kujiunga na shule nitakapokuwa shuleni. Ninaahidi kufuata kanunui na taratibu za shule na kutii maelekezo ya viongozi wangu ili kupata taaluma bora na maadili yanayotakiwa.
3. Ninaahidi kwamba sitajihusisha katika ushawishi, kuchochea au kushiriki kwa namna yeyote katika mgomo au fujo katika muda wote wa uanafunzi wangu; nikiwa ndani au nje ya shule.
4. Ninaahidi kwamba sitajihusisha katika makosa yeyote ya kijinai kwa namna yeyote ile.
5. Ninaahidi kwamba nitashirikiana vizuri na walimu, wafanyakazi wengine na wanafunzi wenzangu kulinda heshima ya shule na Taifa kwa kuwa na nidhamu nzuri na kujitahidi katika masomo ili niweze kupata matokeo mazuri kwenye mitihani.
6. Nipo tayari kuchukuliwa hatua za kinidhamu endapo nitakiuka taratibu zilizoelekezwa.

Saini.................................. Tarehe........................

**KIAMBATISHO C (Jaza na irudi shuleni)**

**FOMU YA UTHIBITISHO WA MZAZI**

1. Mimi mzazi/mlezi wa .........................................nimesoma maagizo, sheria pamoja na taratibu zote za shule. Ninaahidi kumsimamia vizuri mwanangu ili aweze kufuata maagizo, sheria na taratibu hizo.
2. Naelewa kwamba uvunjaji wowte wa maagizo, sheria na taratibu za shule utamsababishia mwanangu kuchukuliwa hatua za kinidhamu.
3. Ninaahidi kwamba nitampatia mwanangu mahitaji yote muhimu ya shule ikiwa ni pamoja na kufuata maelekezo mengine yatakayotolewa.
4. Ninaahidi kwamba nitashirikiana na walimu na uongozi wa shule kuhakikisha kwamba mwanangu anakuwa na nidhamu nzuri na anafanya vizuri kitaaluma.
5. Ninaahidi kufuatilia maendeleo ya mwanagu kitaaluma ikiwa ni pamoja na kumkagua mazoezi anayopewa shuleni.

Saini.................................. Tarehe........................